

Mume mzee



✎ Aranya
☑ Sunniva Høiby-Øiset
📄 Jacob Haule
|| 5
😊 Kiswahili! MS



LIDA Stories

lidastories.net

Mume mzee

✎ Aranya
☑ Sunniva Høiby-Øiset
📄 Jacob Haule




This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0).
<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0>




Nilifikiri wanaume wa Norwei ni wanaume bora duniani, lakini hii si kweli! Kabla sijaonana na mwanaume ambaye alikuja kuwa mume wangu, nilikuwa ninafanya kazi kiwandani Bangkok na yeye aliishi Pattaya. Tulikutana mtandaoni na hatimaye tukawa wapenzi.

Baada ya muda tukaamua kuoana.
Ninatoka katika familia maskini, kwa hiyo
kuwa na mume kutoka nchi nyingine
ambaye atahudumia familia yangu ilikuwa
ni miongoni mwa sababu za kuolewa nae.






Tuliamia Norwei na nilianza kwenda shule kujifunza Kinorwei. Ulikuwa ni wakati mgumu sana. Sikuwa na leseni ya udereva na mume wangu akawa ananipeleka shuleni, ananisubiri na ananirudisha nyumbani. Ilikuwa ni umbali wa saa moja. Baada ya muda, tuliamia karibu lakini alisisitiza kuendelea kunipeleka shuleni. Hakutaka nitembee peke yangu.




Sikuwahi kuwa na pesa tangu nihamie
 Norwei. Mara moja, mume wangu alinipa
 pesa kwa ajili ya chakula cha mchana lakini
 kwa sababu ni pesa kidogo, niliweka
 kando. Rafiki zangu shuleni walitaka
 kunisaidia nipate kazi lakini mume wangu
 alisema haiwezekani. Hatifikirii kama
 kufanya kazi ya usafi ni kazi inayokubalika
 kwangu.



Sielewi hata itakuwaje, mpango wangu ni
 kwenda shule nyingine lakini mume wangu
 hapendi nifanye hivyo. Ana mpango wa
 kuniongeza ugumu. Ninataka kupinga
 lakini sijui nafanyaje, si rahisi kuishi katika
 nchi ya ugenini na mume mzee kama
 nilivyofikiri.



Badala yake, alinitafutia kazi nyingine, kujenga gereji. Alikuwa boshi na nilifanya kila kitu. Alikuwa hawezi kufanya makubwa kwa sababu alikuwa mgonjwa. Hakuwahi kunipa pesa aliyoipata kutokana na kazi ya kujenga gereji.



Siku moja alisema kuwa anahisi upweke akiwa peke yake nyumbani. Kwa hiyo, tuliamua kuwa na mbwa. Sikutaka mbwa kwa sababu nilikuwa nimechoka baada ya kutoka shule na nilikuwa na kazi nilizopewa nizifanye nyumbani. Alisema ataweza kumtembeza mbwa kila siku lakini mwishowe nililazimika kuwahudumia wote, mbwa na mume wangu mzee.